

CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM
S. L. P. 35091 DAR ES SALAAM - TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

**MATUMIZI YA MFUMO WA KIELEKTRONIKI WA KUKUSANYA
MAPATO YA SERIKALI (GePG)**

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere Mlimani, kinapenda kuwataarifu wanafunzi, wafanyakazi, wadau mbalimbali na umma kwa jumla kuwa kuanzia tarehe 1 Februari 2019 malipo yote yatapokelewa kwenye Akaunti za Chuo kupitia Namba Maalum ya Kumbukumbu (*Control Number*).

Wanafunzi watahitajika kuomba Namba Maalum ya Kumbukumbu (*Control Number*) kupitia Mfumo wa ARIS na wasio wanafunzi watahitajika kuwasiliana na Ofisi ya Msarifu kwa ajili ya kupata Namba Maalum ya Kumbukumbu ya malipo husika.

Baada ya kupata Namba Maalum ya Kumbukumbu (*Control Number*) malipo yote yafanyike kupitia Benki za CRDB, NMB na NBC kwa akaunti zifuatazo:

NA	BENKI	JINA LA AKAUNTI	TAWI	AKAUNTI NAMBA	AINA YA FEDHA
1	CRDB	UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM	UDSM	0150329567500	TZS
2	CRDB	UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM	UDSM	0250329567500	USD
3	NMB	UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM	UNIVERSITY	20810006388	TZS
4	NMB	UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM	UNIVERSITY	20810006390	USD
5	NBC	UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM	UDSM	040139000020	TZS
6	NBC	UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM	UDSM	040105002444	USD

Unaweza pia kulipa kwa kutumia simu ya mkononi kama ifuatavyo:

- Fungua Menu ya Mpesa, Tigo Pesa, Airtel Money, Ezy Pesa, T-Pesa (TTCL Pesa) au Halopesa
- Chagua "Lipa Bill" na Mpesa, Tigo Pesa, Airtel Money, Ezy Pesa, T-Pesa (TTCL Pesa) au Halopesa
- Chagua Malipo ya Serikali
- Ingiza Namba Maalum ya Kumbukumbu ya Malipo (*Control Number*) yako
- Ingiza kiasi unacholipa
- Ingiza namba ya siri
- Thibitisha malipo

Tafadhali Zingatia:

Namba yako ya siri ya simu ni siri, usimpe wala kumuonyesha mtu yeyote.


Jihadhari na matapeli, kwa maswali na ufafanuzi zaidi tafadhali fika ofisi ya Msarifu au Mamlaka husika za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, au wasiliana nasi kwa mawasiliano yafuatayo:

Simu ya Mezani: +255 22 2410715

Barua Pepe: bursar@admin.udsm.ac.tz

Tovuti: <http://www.udsm.ac.tz>

Imetolewa na



Prof. David A. Mfinanga

NAIBU MAKAMU MKUU WA CHUO - UTAWALA